*Taarifa kuhusu*

# Dhuluma za kijinsia na jinsi ya kupata msaada




## Toleo la Pili

MIDRIFT HURINET
Haki Kwa Wote

DIGNITY
DANISH INSTITUTE AGAINST TORTURE

*Wakati mwingine vurugu zinapozuka nyumbani, mwanamke hufukuzwa pamoja na watoto na mwanaume hafuatilii ustawi wa watoto. Hii inawafanya baadhi ya wanawake kuendelea kuishi katika mahusiano ya unyanyasaji.*

Chifu

*Nilibaki kwa uhusiano, kwa sababu ya utamaduni na vitisho. Kisha, akanifukuza mimi na watoto baada ya kujifungua. Nimepata msaada kupitia kujitolea kwa Daktari mashinani na ninaishi bila vurugu zake na watoto wangu.*

Muathirika wa dhulma za kijinsia

## Dhuluma za kijinsia ni nini?

Dhulma za kijinsia zinazoelekezwa dhidi ya mtu kwa sababu ya majukumu ya kijamii au kitamaduni yanayohusiana na kuwa Mwanamke au Mwanaume. Ni ukiukaji mkubwa wa haki ya kibinadamu, bila kujali wakati, wapi, au jinsi inavyofanyika.. Inaweza kuathiri wanaume, wanawake na watoto: Dhuluma za kijinsia huchukua aina nyingi:



## Dhuluma za kimwili

Kitendo chochote kinachosababisha madhara ya mwili kwa mfano kusukuma, kupiga, kupiga kofi, shambulio.

## Dhuluma za kisaikolojia / kihisia

Kitendo chochote kinachosababisha matatizo ya akili au madhara kwa mtu binafsi kwa mfano udhalilishaji, matusi, vitisho, kupunguza mawasiliano na wengine, udhibiti wa kifedha, kuzuia upatikanaji wa wa huduma za matibabu au huduma nyingine.





Kuripoti vurugu za washirika wa karibu[1] hasa miongoni mwa wanaume hukutana na kejeli kutoka kwa watu katika jamii. Tazama **uk 13** kwa njia salama ya kuripoti.

## Dhuluma za kijinsia

Kitendo chochote cha ngono au jaribio lililofanywa dhidi ya mtu bila idhini yake, kwa kulazimishwa au kutumia nguvu na mtu yeyote bila kujali uhusiano wao na muathirika kwa mfano, ngono ya lazima, ubakaji, vitendo kama mguso usiofaa.



1 Vurugu za washirika wa karibu ni unyanyasaji wa nyumbani na mpenzi



Mtu yeyote anaweza lengwa na unyanyasaji wa kijinsia, hata hivyo, utafiti unaonyesha wanawake na wasichana mara nyingi wana uwezekano mkubwa wa kuathiriwa.Takwimu kutoka kwa Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya ya Kenya (KDHS, 2022) zinaonyesha kuwa **zaidi ya 40% ya wanawake wa Kenya wamepata angalau sehemu moja ya unyanyasaji wa wenzi wa karibu.**

Unyanyasaji wa wapendanao (kwa mfano mume, mke, mpenzi), ni moja ya aina za unyanyasaji zinazojulikana kuathiri wanawake, wanaume na watoto wao.

*Mifano mingine ya dhuluma ni kama:*

- **Ukeketaji (FGM)** - kuondolewa kwa sehemu au jumla ya sehemu za viungo vya uzazi vya kike kwa sababu zisizo za kimatibabu.



MIDRIFT HURINET
Haki Kwa Wote

- **Dhuluma za kiuchumi** - ni udhibiti wa rasilimali za kifedha na mpenzi kwa mfano kumnyima mwenzi wako kufanya kazi wakati wanataka. Utafiti wa hivi karibuni (MIDRIFT & DIGNITY, 2022) pia unaonyesha kuwa dhuluma za kiuchumi ni pale mtu anapokataa kutoa mahitaji ya msingi kwa familia wakati anaweza.

- **Ndoa za mapema** - ni ndoa yoyote ambapo angalau mmoja wa wanandoa ni chini ya umri wa miaka 18. Ni aina ya ndoa ya kulazimishwa, kutokana na kwamba moja au pande zote mbili hazijaonyesha idhini kamili.

## Ni nini kinachoweza kusababisha dhuluma za kijinsia?


Kulingana na utafiti wa dhuluma za kijinsia (MIDRIFT & DIGNITY, 2022), unyanyasaji wa kijinsia unasababishwa na: imani za kitamaduni na kukubalika kwa dhuluma, vizuizi katika kuripoti dhuluma za kijinsia na kutopata haki, kufanya dhuluma ionekane kawaida kati ya wapendanao na kanuni za kijinsia.

### *Hatari ya dhuluma inaweza kuongezeka ikiwa mtu:*

- Ameshuhudia au kulelewa katika mazingara ya dhuluma.
- Kiwewe (trauma).
- Wanaishi katika hali ngumu na viwango vya juu vya mafadhaiko na umaskini.
- Wakati sababu za msingi za vurugu hazishughulikiwi
- Utumizi mbaya wa pombe na/au madawa ya kulevya.

## Vizuizi vya kuripoti kesi za Dhuluma za kijinsia

- Vizuizi vya miundo (kwa mfano ngazi zinaweza kuathiri watumiaji wa kiti cha magurudumu, ukosefu wa nafasi salama za kuripoti, ukosefu wa usiri, umbali wa kupata huduma)
- Vizuizi vya kimawasiliano (kwa mfano lugha, ukosefu wa habari juu ya taratibu za kuripoti)
- Vizuizi vya kawaida kama unyanyapaa, kejeli na ubaguzi kutoka kwa watu.
- Vizuizi vya kimfumo (kifedha, uhifadhi duni wa ushahidi, vitisho na vitisho kwa waathirika au mashahidi).




Ni muhimu kutilia maanani na kuangazia mahitaji ya watu wenye ulemavu (Kimwili, kusikia na kuongea, ulemavu wa kuona na kiakili) ili kuhakikisha wanaweza kupata huduma.




*Je, unajua kwamba unaweza ondolewa ada ya fomu ya P3[2] hospitalini?*

2 Fomu ya P3 ni hati ya kisheria iliyotengenezwa kwa kesi za korti za shambulio na/ au ubakaji. Fomu za P3 zinapatikana bure mtandaoni. Katika kituo cha polisi ada inatozwa kwa kuchapisha. Ada za uchunguzi wa kimatibabu zinatozwa hospitalini.

## Kutatua kesi kinyumbani



- Mahakama za Kangaroo[3] sio vikao halali kwa kusuluhisha dhuluma za kijinsia.
- Tunahimiza jamii kusuluhisha dhuluma za kijinsia kisheria.

## Watoto na dhuluma za kijinsia

- Watoto wako katika hatari ya kudhulumiwa kijinsia na kutelekezwa na wazazi.
- Tuwaelimishe watoto juu ya elimu ya ngono inayowafaa na maana ya idhini.
- Tengeneza nafasi salama kwa watoto kuelewa na kuzungumzia mipaka kuhusu ngono pia jinsi ya kuripoti unyanyasaji.
- Kuhakikisha wanaodhulimu Watoto wanachukuliwa hatua za kisheria.




[3]Mahakama isiyo rasmi inayoshikiliwa na kundi la watu katika jamii. Mchakato haujumuishi ushahidi na unaweza kupuuza mchakato unaostahili na kufikia hitimisho lililoamuliwa mapema.

## Je, unyanyasaji wa kijinsia unaweza kuathiri vipi afya ya mtu?

Dhuluma za kijinsia zinaweza kusababisha majeraha makubwa ya kimwili na wakati mwingine hata kusababisha kifo. Inaweza kuwa na madhara ya muda mrefu ya afya ya ngono na uzazi ikiwa ni pamoja na magonjwa ya zinaa, fistula, mimba zisizopangwa (hatari na kuavya mimba kwa njia isiyo salama) pamoja na matatizo ya mimba.

Licha ya madhara ya afya ya kimwili, dhuluma pia zinaweza kuathiri sana ustawi wa akili wa waathirika na wanafamilia wao. Inaweza kusababisha:

### Msongamano wa mawazo - ina dalili kama vile:

- Uzoefu wa mafadhaiko, "kuwa na mawazo mengi" au wasiwasi
- Kuwa na hofu
- Kutokuwa na utulivu au tahadhari
- Maumivu mwilini
- Ukosefu wa usingizi
- Ongezeko la mpigo wa moyo



## Kutokuwa na matumaini au kutofurahi - ina dalili kama vile:

- Hisia za huzuni na kuhisi ganzi
- Kupoteza hamu ya kula au kula sana
- Kupoteza maslahi au kujiondoa kutoka kwa kazi au shughuli unazofanya
- Kujitenga na kujiondoa kwa wengine, kuhisi upweke au kutengwa na wengine na kutoshiriki kama kawaida katika familia na jamii

**Kukabiliwa na dhuluma za kijinsia pia kunaweza kusababisha unyanyapaa na aibu kutoka kwa familia na jamii Ikijumuisha:**

- Kulaumu muathiriwa kwa kusababisha dhuluma kwa mfano kutokuwa mpenzi mzuri  na anastahili dhuluma kama nidhamu, ubakaji (kwa mfano kuwalaumu wanawake kwa kubakwa
- Kujilaumu kwa dhuluma kwa mfano waathiriwa wanahisi kuwa ni kosa lao wenyewe kwamba wanapitia dhuluma.
- Kukosekana kwa msaada  wa kijamii

Unyanyapaa na lawama pia hutokea kama muathiriwa anachagua kukaa katika uhusiano wenye dhuluma.**Kwa lolote lile, dhuluma kamwe si kosa la muathiriwa.**



## Unaweza kupata wapi msaada katika jamii?

Ikiwa umepitia dhuluma za kijinsia, unaweza kupata msaada kwa:

**Vituo vya Afya vya Kaunti**

Watu wa mawasiliano:

- Afisa wa Kliniki
- Wafanyakazi wa ugani wa afya ya jamii (CHEW)
- Wahudumu wa afya ya jamii wa kujitolea (CHVs)

**Nairobi Women's Hospital kote nchini**

Wasiliana:

- Mshauri wa kisaikolojia

**Hospitali ya Level 5:**

- Gender-Violence Recovery Centre (GVRC)
- The Youth-Friendly Centre

**Hospitali ya Level 4:**


- Youth-Friendly Centre

**Vituo vya polisi**

- Afisa anayeshughulikia maswala ya kijinsia (Gender desk)
- Vituo vya uokoaji (Rescue centers)

## Unaweza kupata wapi msaada/ushauri?

Wakati mwananchi anapitia dhuluma za kijinsia, anaweza kupata huduma kama vile: Ushauri wa bure, msaada wa kisheria, huduma za uokoaji na huduma za ulinzi wa watoto. Simu zote zilizoorodheshwa ni bure na za siri.



Unaweza pia kuwasiliana na huduma zifuatazo :

**Healthcare Assistance Kenya(HAK)**
**Gender-Based Violence Hotline**
**Simu ya mkononi:** 1195 (Bila Malipo)

Nambari ya simu imeunganishwa na vituo vinavyotoa matibabu na kuzuia maambukizi ya ugonjwa ya zinaa, msaada wa kisheria na vituo vya uokoaji. Pia hutoa huduma ya siri ya ushauri kwa masaa 24. Ushauri wa simu na uratibu wa shughuli za uokoaji kupitia mfumo wa SMS kwa waathiriwa.

**Police Gender Based Violence Hotline**
**Simu :** 0800730999 (Bila Malipo)

**Liverpool VCT one2one youth Hotline**
**Simu :** 1190 (Bila Malipo)
www.lvcthealth.org

Vijana wanapata ujumbe za bure juu ya ngono
Afya ya uzazi na haki

**Aunty Jane Hotline**
Simu ya mkononi : 0800-721530 (Bila Malipo)
www.aunt jane.org

Taarifa juu ya afya ya uzazi na ngono.

**MIDRIFT HURINET**
**Rufaa ya watoa huduma husika**
**Tel** : 0702-520894 (Kwa Malipo)



## Unaweza kupata wapi msaada ?




Zungumza moja kwa moja na mshauri au mhudumu wa afya ya kijamii. Unaweza pia kuzungumza na mtu unayemwamini kama jamaa, familia au rafiki.

Waathiriwa wanaweza kujiunga na kikundi cha msaada ili kushiriki na waathiriwa wengine. Tiba ya kikundi husaidia uponyaji na kukabiliana na dhuluma za kijinsia. **Afya ya akili na ustawi wa waathiriwa wa dhuluma ni muhimu**






*Huduma za ushauri zilinisaidia kutafakari juu ya maisha yangu na kufanya maamuzi muhimu ambayo yalinikomboa kutoka kwa uhusiano wangu wa zamani wenye uchungu. Kwa sasa niko imara katika kudhibiti maisha yangu.*

Muathiriwa wa dhuluma ya kijinsia

# Vidokezo vitano vya kusaidia mtu anayekabiliana na dhuluma za kijinsia

1. Kamwe usimlaumu muathiriwa kwa kile kilichotokea- sio kosa la muathiriwa.
2. Kuwa wa msaada kwa muathiriwa yaani, kwa kumsikiliza kwa makini
3. Wasiliana mara kwa mara na muathiriwa ili kuangalia ikiwa yuko salama. Katika mawasiliano yenu, hakikisha ni kwa njia salama ambapo mnyanyasaji hawezi kufuata mawasiliano.
4. Epuka kueneza uvumi au kuwaambia wengine kuhusu dhuluma bila idhini kutoka kwa muathiriwa.
5. Muathiriwa akihitaji msaada zaidi, mwelekeze mahali atapata msaada katika jamii.

MIDRIFT HURINET
Haki Kwa Wote


*Maelezo ya mawasiliano*

**Barua pepe :** info@midrifthurinet.org
**Simu ya mkononi :**+254 254 700 423 262

**NAKURU**
**Address:** Christ The King Training Institute Building, 1st Floor, Nakuru
Ronald Ngala Rd ,
P.O Box 16326-20100 ,Nakuru, Kenya

**NAIROBI**
**Address:** Tetu Apartments, Door 4, Ralph Bunche Rd, 2nd Floor
Milimani Ln,
P.O Box 11128-00100. Nairobi ,Kenya